➢ Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
➢ Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali zetu,
➢ Maafisa wengine kutoka pande zote mbili,
➢ Mabibi na mabwana Waandishi wa habari,

1. Ningeomba tushirikiane kwanza kumushukuru Mwenyezi Mungu, aliyetuwezesha kufika hapa na kutukutanisha katika nchi hii nzuri ya Tanzania.

➢ Mheshimiwa Rais,

2. Niruhusu tena nitoe shukrani zangu za dhati
kwa kunialika kuja kuyitembelea nchi hii ndugu na nzuri ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Tunawashukuru sana kwa mapokezi ambayo tumepewa, mimi pamoja na ujumbe wangu, tangu tuingie nchini.
Tunakushukuru kwa ukarimu mkubwa, Mheshimiwa Rais.

➢ Muheshimiwa Raisi,

3. Mwezi wa saba, mwaka huu, ulitembelea nchi yetu ya Burundi. Tulikuwa na mazungumzo ya faraha, mazungumuzo yenye matumaini, kuhusu namna ya kudumisha zaidi na zaidi, uhusiano kati ya nchi zetu mbili.
Tulizungumzia pia mbinu za kuinua uchumi wetu, ikiwemo miradi ya mawasiliano kwa sekta mbalimbali ikiwemo na sekta ya miundombinu.

4. Siku ya leo, tumekuja kutimiza methali ya Kirundi, lugha ya kitaifa nchini Burundi, isemayo kuwa AGAFUNI KABAGARA UBUMWE NI AKARENGE.
Ikimanisha kwamba…jembe linalopalilia ushirikiano ni mguu.
Yaani kutembeleana mara kwa mara bila kuchoka.

Na muhimu zaidi, pia nimekuja hapa kukupongeza na kukumpa moyo dada yangu, kwa mfano mzuri wa uongozi bora na maendeleo unaonyesha duniani na Afrika kwamba kinamama, licha ya shida ulioanza nayo ya kumpoteza shujaa wa sisi sote Hayati John Pombe Joseph Magufuli.
Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema huko peponi.

➢ Dada yangu raisi,
➢ Waheshimiwa
➢ Ndugu Waandishi wa habari,

5. Tumekuja kudumisha ushirikiano wa kipekee, urafiki, undugu na ujirani mwema uliopo kati ya Serikali zetu na wananchi wetu kwa jumla.
Burundi na Tanzania tuna muelekeo mmoja, na tunashirikiana kwenye Nyanja za kisiasa na kiusalaama, ndani ya Jumuiya ya Africa Mashariki, ndani ya Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Maziwa Makuu, ICGRL, ndani ya Umoja wa Africa (AU), hata kwenye ngazi za Kimataifa (UN).

Hapa, nikubaliye, Mheshimiwa Rais, nizitowe pongezi zangu kwa nchi ya Tanzania kwa juhudi zake zisizokuwa na mfano katika kuimarisha Jumuia ya Afrika Mashariki na jinsi inavyojitolea ili ihakikishe Jumuia yetu imefikiya malengo yake.

Kwa upande mwengine, Serikali ya Tanzania imeahidi kuiunga mkono serikali ya Burundi kuwa mwanachama wa SADEC na kuziomba nchi ambazo ziliwekea Burundi vikwazo vya kiuchumi kuviondowa.

Juhudi za kidiplomasiya zinaendelea ili vikwazo hivyo viondolewe kabisa.
Na ushirikiano huo una mizizi ya kutokea mbali tangu enzi za mababu zetu:

➢ Mashuja wetu Hayati Ludoviko Rwagasore na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, bega kwa bega, walipigania uhuru wa nchi zetu myaka ya sitini.

➢ Tanzania iliwahifathi karibu milioni ya wanachi wa Burundi, wakikimbia machafuko yaliokuwepo nchini kwetu tangu myaka ya sitini, na sabinini na mbili

➢ Na hivi karibuni, mwaka wa elfu mbili na kumi na tano wakati wa jaribio la kuipinduwa serekali ya Hayati NKURUNZIZA, Tanzania ilisimama kidete upande wa serikali ya Burundi .

Akhsanteni saana Watanzania kwa mchango wenu na musije mukalegeza msimamo, kwani aluta continua.

6. Tunawutambuwa kwa namna ya pekee mshikamano, Serikali ya Tanzania na wananchi wa Tanzania kwa jumla, mliotuonyesha nyakati hizo ngumu zilizotufikia nchini Burundi. Mwenyezi Mungu awarudishie maradufu.

7. Tunamshukuru Mungu, inchi ya Burundi imefufuka kisiasa, kiusalama, kijami na kiuchumi. Idadi ya warundi wanaorejea nyumbani kutoka uhamishoni, ni ushuhuda mkubwa kwamba Amani na utulivu vinatawala inchini.

8. Kwa fursa hii, napendelea kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta, Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Museveni bila kusahau Jumuia yetu ya Afrika Mashariki kwa juhudi zao.
Vile vile tunamshukuru Mungu kwa kuskia maombi yao ambayo yalipelekea vikwazo hivyo kupunguwa na kuelekea kutoweka kabisa.

➢ Ndugu Waandishi wa habari,

9. Kumbukeni kwamba ziara yangu ya kwanza nchini Tanzania niliifanya mnamo mwezi Septemba mwaka 2020, na kukutana na Marehemu Rais, Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, katika mji wa bandari wa Kigoma.
Ziara zote mbili, (leo na ile ya Kigoma) zinalenga kudumisha fani ya kidiplomasia na uchumi.

10.Hapa nitataja mifano michache pekee:

❖ Upande wa Burundi, nchi bado haijasonga mbele katika sekta ya madini; iko tayari kujifunza utaalam wa Tanzania katika sekta hii, na hati ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya madini tayari imesainiwa.
Burundi hivi karibuni itaanza kuagiza mkaa wa mawe kutoka Tanzania ili kuendeleza tasnia yake ya chuma;

❖ Nchi zetu mbili zimekubaliana kuhusu njia ya kufadhili kazi za ujenzi wa reli ya Uvinza-Musongati na kazi zinaweza kuanza hivi karibu;

❖ Serikali ya Burundi tayari imeanza kazi ya kukarabati na kuifanya ya kisasa Bandari ya Bujumbura, ambako kumetengwa sehemu ya ujenzi wa meli. Baada ya kuhitimishwa kazi kwenye Bandari hiyo ya Bujumbura, usafirishaji wa bidhaa na watu kati ya Bujumbura, Kigoma, na Mpulungu nchini Zambia bila kusahau

Kalemie nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo; itakuwa rahisi sana tena kwa bei nafuu;

❖ Kazi za ujenzi wa barabara ya Mugina-Nyanza Lac zimekamilika, wakati zile zilizo kwenye barabara ya Nyanza Lac-Rumonge-Gitaza zimeanza hivi karibuni.

Sehemu ya Gitaza Bujumbura haitachukua muda mrefu kujengwa pia. Barabara hii itapunguza umbali na gharama za wasafiri wa malori ambao wanapaswa kufanya mtaro mrefu kwa sababu sehemu zingine za barabara ya Mugina na Bujumbura hazipitiki;

❖ Serikali ya Burundi inashukuru sana Serekali ya Tanzania kwa kuhaidi maeneo mawili kwa ujenzi ya Bandari Kavu, ambayo itaruhusu kupunguzwa kwa gharama za usafirishaji na faini kwa wale bishara zao zitazidi muda katika Bandari ya Dar Es Salam;

❖ Kama sehemu ya ushirikiano katika sekta ya kilimo, Burundi iliiomba Tanzania kuipatia ardhi inayofaa kulima karibu na mpaka ili kuongeza mazao yake ya miwa, na hivyo kuongeza uzalishaji wa sukari. Tungependa kutoa ombi kama hilo kwa mazao mengine ambayo yatawanufaisha raia wa nchi zote mbili;

❖ Kuhusu vita dhidi ya janga la Covid-19, tunafurahishwa na mafanikio yaliyorekodiwa katika kampeni yetu kote nchini. Burundi imeweka kipaumbele hatua za kiafya, hasa kuwataka raia kutosogeana, na upimaji ili mara tu baada ya kuambukizwa, mgonjwa atibiwe nyumbani na baada ya kupona, anaweza kufanya shughuli zake za kila siku. Tunajivunia pia kuwa juhudi za pamoja za nchi zetu mbili zimefanya uwezekano wa kuacha mipaka yetu ya

pamoja wazi, na kwa hivyo kuendelea na biashara wakati ambapo majirani zetu wengi walikuwa wamefunga raia majumbani kwao ;

❖ Mwishowe, kampuni ya Burundi ya Fomi-Itracom inayotengeneza mbolea za madini tayari imewasili nchini Tanzania na itaajiri wafanyikazi wa Burundi na watanzania kwa usawa. Tanzania itanufaika sana kwa swali la uagizaji mbolea litatoweka na pesa zilizookolewa zinaweza kuwekezwa katika sekta zingine.

➢ Ndugu Wandishi wa habari,

10. Huu ni ushuhuda kwamba wafanyabiashara wenye busara, Burundi na Tanzania wanasafiri kwa mashua moja, ingawa uboreshaji unahitajika hapa na pale. Nanufahika na fursa hii ili kuwatolea wito wawekezaji wengine kuanzisha biashara zao katika nchi zetu hizi mbili.

11. Kwa kuitimisha, napendelea kumfahamisha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na raia wote wa Tanzania kwamba, tunaishukuru kikamilifu nchi ya Tanzania kwa kukubali kubeba mzigo wa kuwakaribisha, kuwapokea kwa mikono miwili warundi tangu miaka ya sitini (60s), wakati wa mauaji ya 1972 na 1993 ; na kuwarahisishia wakimbizi wanaohitaji kurejea nchini toka amani iliporejea nchini Burundi. Ifahamike kuwa zaidi ya laki 2 (200.000) kati yao walipewa uraia zama za utawala wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete; sasa wana haki kamili kama Raia wa Tanzania.

12. Kabla sijamaliza, niseme machache kuusu usalama. Upande wa usalama : ushirikiano mzuri uliopo kati ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwenye mipaka yetu ni wa kuridhisha. Haya ni Matunda ya ujirani mwema na kupashana habari kati ya viongozi wetu na wananchi wetu waishio mpakani.

Pamoja na hali tulivu hio, kuna kundi linaloongozwa na Mwana siasa Alexis SINDUHIJE ambalo linashilikiana na kundi la terrorism ADF.  Lengo lake kubwa ni  kuyumbisha usalama kwenye inchi za kanda la maziwa makuu. Kinachosikitisha ni kwamba wanaangamiza maisha ya wananchi wasiyokuwa na hatia.

13. Mwisho kabisa, ninatoa tena shukrani zangu za dhati kwa Dada yangu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Ndugu raia wa Tanzania. Ujumbe wangu, na mimi, tumepokelewa kwa ukarimu usio na kifani. Kama tunavyopenda kusema, watanzania sio marafiki tu, bali ni ndugu zetu.

➢ Ndugu zangu watanzania,

14. Siku chache tu nilizokaa Dar es Salaam, nilijifunza kwamba umoja ni nguvu na utengamano ni udhaifu. Na nyumbani, tunasema kwamba tukiwa pamoja tunaweza. Watanzania na Warundi wakishirikiana, na sisi tukishirikiana kama viongozi, bilashaka tutaweza, I can assure you.

Mwenyezi Mungu ayilinde Tanzania

Mwenyezi Mungu ayilinde Burundi

Asanteni.